MRADI WA KIMATAIFA WA KIFEMINIA
MAFUNZO LINGANISHI YA NCHI MBALIMBALI YA
HARAKATI YA WANAWAKE NA JINSIA
NA USOMI

NCHI: TANZANIA

Jina la Mhojiwa: Nasra Juma Mohamed

Jina la mhojaji: Anneth Meena

Mahali: Unguja, Zanzibar

Tarehe: 3/28/2023

Chuo Kikuu cha Michigan
Taasisi ya Utafiti wa Wanawake na Jinsia
1136 Lane Hall Ann Arbor, MI 48109-1290
Simu: (734) 764-9537

Barua Pepe: um.gfp@umich.edu
Tovuti: http://www.umich.edu/~glblfem

© Regents of the University of Michigan, 2023

Nasra Juma Mohamed ni Mkurungezi msaidizi msaafu wa Idara ya uhamiaji Tanzania. Alitumikia idara ya uhamiaji akiwa na wadhfa mbal mbali kwa kipindi cha miaka takribani 41. Akiwa katika kitengo hicho, Bi. Nasra alikuwa pia ni mwanamichezo, vile vile ni kocha wa mpira wa miguu kwa wawnawake aliyeidhinishwa na baraza la mpira wa miguu (FIFA). Aliweza kuvunja vizuizi katika michezo inayotawaliwa na wanaume na vile vile kutamani kupunguza kanuni na tamaduni zilizoeleka za wanaume kufundisha wanawake na wasichana mpira na badala yake wanawake zaidi wanaingia katika hii tasnia ya michezo na kufundisha mpira.

Bi. Nasra alianzisha team ya kwanza Zanzibar ya wanawake ya mpira mwaka 1988 ambayo ilijulikana kama Women's Fighers. Katika kipindi cha mwaka 2007 filamu ndogo ilitengenezwa ikijulikana kama Malkia wa Soka Zanzibar iliyoonesha changamoto wanazopitia wanawake kama Bi. Nasra katika kukuza na kuanzisha timu za jinsi ya ke. Filamu hiyo ilifikia vigezo na kuonyeshwa kwenye Tamasha la Filamu la Kimataifa la Zanzibar. Filamu hii Ilileta uthibitisho na umakini mzuri kwenye vyombo vya habari.

Bi. Nasra ameshika nafasi mbalimbali katika tasnia ya michezo hii ikiwa ni pamoja na kuteuliwa kuwa mjumbe mtendaji wa kamati ya olimpiki ya Tanzania (2003 - mpaka sasa); Kocha Mkuu ya timu ya wanaume ya daraja la kwanza - Klabu ya Kikwajuni ya mpira wa miguu Zanzibara (2021 mpaka sasa); Mwenyekiti wa kamati ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (2011 - 2020); Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake Twiga Stars (2014 - 2016); na Kocha Mkuu wa timu ya soka ya daraja la kwanza ya Uhamiaji (2016 - 2020).

Bi. Nasra alianza michezo tangu utotoni. Alicheza mpira wa vinyoya kwenye nafasi tofauti tofauti na kuchinda makombe mbalimbali kama vile Michuano ya Kwanza Afrika ya Mpira wa Vinyoya yaliyofanyika Kumasi nchini Ghana (1979); Michuano ya Pili Afrika ya Mpria wa Vinyoya yalifanyika Beira nchini Msumbiji (1981); Michuano ya Jumuiya ya Madola ya Mpira wa Vinyoya yalifanyika Brisbane, nchini Australia (1982); Michuano ya Africa ya Mpira wa Vinyoya yalifanyika Beira nchini Msumbiji (1984); Michuano ya Tano ya Mpira wa Vinyoya Lagos nchini Nigeria (1988); na Michuano ya Nchi za Kundi la Mabingwa wa dunia ya Mpira wa Vinyoya yalifyanyika nchini Hong Kong (1993). Baadaye aliingia kwenye mpira wa miguu baada ya viwanja vya michezo ya mpira wa vinyoya kubomelewa Zanzibar na hivyo kuanza kucheza mpira wa miguu na wavulana.

Bi. Nasra ameshika nyandhifai mbalimbali katika tasnia ya michezo: kwa mfano, Timu ya taifa ya mpira wa miguu ya ya wanawake (2001 - 2003); Manager wa Timu kwenye michezo ya Jumuiya ya Madola ya XIX yaliyofanyika nchini India (2010); Kocha Msaidizi Michuano ya Afrika kwa Wanawake (2012 - 2013);Kocha Msaidizi kwenye Michuano ya Afrika ya Wanawake (2012 - 2013); Kocha Msaidizi ya Afrika kwa Wanawake yaliyofanyika nchini Zambia (2014 - 2015); Kocha Mkuu Michuano ya Afrika kwa Wanawake yaliyofanyika nchini Zimbabwe (2015 - 2016); Meneja Mkuu wa Timu kwenye Michezo ya Jumuiya za Madola Tanzania (2018).

Bi. Nasra amechukua kozi mbalimbali za michezo. Amefuzu na leseni ya kufundisha mpira wa miguu; anacheti cha usimamizi wa michezo; stashahada katika mahusiano ya nje na

diplomasia (2005 - 2006), na shahada katika kazi ya jamii kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2017 - 2020).

Anneth E. Meena, alizaliwa 1971, ni mtafiti, mwanaharakati na mfeminia. Bi. Meena ni mshauri wa kujitegemea kwenye maeneo mbalilmbali ikiwa ni pamoja na mazingira, Afya na maswala ya Jinsia. Amefanya kazi na mashirika mbalimbali kwenye nafasi mbalilmbli ikiwa ni pamoja na mratibu wa ufuatiliaji na tathmini World Vision, ofisi ya Arusha (2000); Mratibu wa mradi wa Kituo vya Ubora na Ufanisi kupitia shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama Jukwaa la Wanaelimu Wanawake wa Kiafrika ambapo program hii ilibobea katika kuzingatia jinsia katika mtaala na ufundishaji unaozingatia jinsia (2001 - 2002). Alikuwa mmoja wa waasisi wa shule ya sekondari ya upili iliyojulikana kama Raida akiwa meneja wa kwanza wa shule na baadaye kuwa mkuu wa chuo cha kati wa kwanza (2007 - 2017). Bi. Meena amefanya kazi kama mshauri wa kujitegema katika mashirika mbalimbali ya haki za wanawake yakiwemo TGNP Mtandao; Mfuko wa Wanawake Tanzania; Soma. Vile vile amefanya kazi za tafiti mbalimbli ikiw ni pmaoja na mabadiliko ya tabia nchi na Taasisi za elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania na Chuo Kikuu cha Michigan, Marekani.

Ms. Meena ni mwanachama wa mitandao mbalimbali kama vile mtandao wa kupinga rushwa ya ngono, mtandoa wa haki ya uzazi, ujinsi na afya.

Bi. Meena ametunukiwa tuzo mbalimbali za kitaaluma ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Hammad kwa kutambua kazi ya kipekee yenye mada ya kimataifa iliyotolewa na shule ya Huduma za Umma ya Wagner, Chuo kikuu cha New York Marekani. Vile vile ni miongoni mwa wanawake wawili wa Africa waliopata udhamini wa masomo kutoka kwa Oprah Winfrey na kusoma katika Chuo Kikuu cha New York, Marekani katika kipindi cha 2004 - 2005. Pia amepokea udhamini wa Ford Foundation na kupata nafasi ya utafiti katika kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Wanawake, Washington, DC, Marekani mwaka 1999. Amepokea tuzo ndogo ya utafiti kutoka Baraza la Maendeleo ya Utafiti wa Sayansi ya Jamii.

Ms. Meena ana shahada ya kwanza katika sayansi ya Mazingira na Jiografia kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town, Cape Town, Afrika ya Kusini (1996). Shahada ya Uzamili ya sayansi ya watu (Demografia) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania (2000); na Shahada ya Sayansi katika Usimamizi wa Huduma za Umma kutoka chuo Kikuu cha New York, New York, Marekani (2005).

Anneth Meena: Okay. Karibu sana mama Nasra kwenye hii session yetu ya leo.

Nasra Juma Mohamed: Asante, asante sana.

AM: Okay. Udahili huu ni sehemu ya mradi wa kimataifa wa kifemenia ambao ni mradi wa kimataifa unaothaminiwa na chuo kikuu cha Michigan. Lengo ni kukusanya taarifa za kihistoria na kuzihifadhi mazungumzo ya wanawake ambapo uharakati wao umechangia kwenye mapambano ya kiwanaharakati na mambo muhimu ya wanawake. Kwa hiyo tutatumia takribani lisaa limoja kujadili maeneo Matano: Maisha yako kwa ujumla na kazi, tafakari yako ya kazi yako, maoni yako kuhusu mahusiano kati ya femenia na harakati na inavyohusiana na kazi yako, mtazamo wako na maoni yako kwenye mtazamo mzima wa takwa la wanawake, mahusiano yako kama yapo, kati ya kazi unayoifanya na hizo za wanaharakati wengine nchini.

Kwahiyo kwa kuanza tuanzie historia ya maisha yako. Unapofikiria kuhusu ulipo leo unaonaje safari yako ilipokufikisha leo, karibu.

NJM: Asante sana Anneth Meena. Kwanza nikushukuru sana, kwa sababu Tanzania tuko wanawake wengi sana mpaka maana yake kufikia watu wengine wakakuona huyu tumuulize, huyu tumsikilize huyu aseme dunia imsikie kwa kweli sio jambo dogo. Sio jambo dogo mimi nawashukuru sana, na kwa kweli maisha yangu mimi tangu nimeyaanza, mimi ni mwanamichezo. Kwa sababu familia yangu ilikuwa na watoto 12 ndugu lakini 12 hao 9 ni wanaume na wote ni wanamichezo. Na mazingira ambayo tunakaa shemeu kabsa ya michezo kwa hiyo tulikuwa na privilege kabsa ya kuwa wanamichezo kwa sababu maeneo ya nyumbani kulikuwa na sehemu ambapo mnaweza kwenda kucheza kwenye hall kucheza indoors games, kwenda kwenye uwanja wa mpira mnazi mmoja pale ambapo kuna uwanja mkubwa sana wa Zanzibar kama unavyo jua kuna piece zaidi ya arobani ndani ya uwanja ule. Kwa hiyo sehemu zote hizo kuna possibilities za kuwa mwanamichezo. Kwa hiyo mimi nashukuru ni mama wa nyumbani kwa sasa hivi, tumezaliwa tukiwa 12 na mimi ni wa pili katika historia yangu ya kuzaliwa na undugu 10 na kaka mmoja na nimesoma mpaka chuo, open University nimechukua degree ya Social work namshukuru mwenyenzi Mungu nimeweza kulifanikisha hilo. Na nimeajiriwa katika idara ya uhamiaji kupitia michezo kwanini nikasema kupitia michezo pamoja na kusoma kwangu nilikuwa katika mashindano ya East Africa ya mchezo wa Band Minten, mimi nimecheza Band minten nimecheza kwenye level ya Tanzania nimecheza kwenye level ya East Africa, nimecheza kwenye level ya Africa, nimecheza kwenye level ya commonwealth game, nimecheza kwenye level ya dunia ya group Series Tanzania imeshiriki kwahiyo mimi nimeshiriki. Kwa hiyo level yangu ya Band minten nilikuwa very high performance utoto wangu na mwaka 81 palifanyika mashindano ya Afrika mashariki na kati kwahiyo bingwa wa Africa kwa mchezo huo kutoka Zimbabwe kipindi kile alikuja Tanzania kushiriki hayo mashindano ya East Africa. Kwa hiyo mimi nilishiriki kwa upande wa Zanzibar tulipoenda kucheza pale Tanzania bara. Na kwa bahati nzuri mimi niseme mimi niliweza kumfunga yule bingwa wa Afrika ambaye aliuchukua ubingwa wa Afrika kama miezi sita nyuma mimi nilichukua ubingwa wa Africa miezi sita nyuma kwa mashindano ambayo mimi nilicheza kama under 18. Na yalifanyika Ghana ilikuwa kumasi Ghana kwa hiyo mashindano yale yalipofanyika mimi nikachukua ubingwa wa watoto yeye yule aliuchukua ubingwa wa wazima senior team. Lakini kwa

sababu alipokuja hapa mimi tayari nilikuwa naweza kuchezea senior team mimi nikapandishwa senior team na kwa Zanzibar nilichezea kama mchezaji tokea Zanzibar senior team kwahiyo kwa bahati nzuri nikaweza kucheza nae na nikamshinda. Sasa mgeni rasmi kwa kipindi kile alikuwa marehemu Raphael Kubaga ambaye alikuwa director wa Immigration department mambo ya ndani. Kwa hiyo baada ya kuniona nimeshinda ule mchezo na mimi nilikuwa kijana mdogo sana alinifuata, akaniuliza unafanya kazi, unasoma au unafanya kitu gani kijana? Nikamwambia nimemaliza mwaka jana tu kusoma, form four ilikuwa nimetangaziwa kwenda kusoma ualimu.Two years nika uchukue diploma ya ualimu kwa hiyo I was hesitating kwa sababu, actually nilikuwa sifeel kwenda kusoma zaidi kwa kipindi kile nilikuwa nataka nifanye kazi. Kutokana na ugumu wa maisha wa familia kwa kweli nilikuwa nahisi nimsapoti baba yangu ambaye kwa kweli alikuwa ni mfanyakazi wa serikali ya mapinduzi Zanzibar kw wizara ya kilimo na misitu kipindi hicho. Lakini maisha yalikuwa magumu sana nyumbani kwa hiyo nilikuwa natarajia kufanya kazi ili tuweze kusapoti nyumbani, excuse me. Sasa, kwa bahati akaniambia mimi nitakuchukua uhamiaji kama umeshamaliza shule na unataka. Nikamwambia ndio, ninataka. “Sisi tunataka champions kama ninyi niwachukue katika idara yangu wa sababu mtaweza perform vizuri na idara yangu itaweza kupata sifa.” Kwa hiyo baada ya week mbili mimi nikafutatwa na idara ya uhamiaji nikaenda kufanya interview na wenzangu na nikachukuliwa katika idara ya uhamiaji. Hiyo ni 81 ya mwezi wa nane, mashindano yalifanyika kama mwezi wa nne hivi. Basi nikaingia uhamiaji nikaenda kusoma polisi college, chuo cha polisi Moshi CCP kwa muda wa miezi kumi na moja. Kipindi kile tulisoma na wa Namibia walikuja kufundishwa uaskari kipindi kile wao walikuwa kwenye harakati wa kutengeneza nchi yao baada ya mambo ya uhuru. Kwa hiyo tukamamliza mimi nikawa kwenye idara ya uhamiaji kwa kipindi chote hicho nikiwa kama ofisa uhamiaji. Mpaka nikafikia kwenye level ya depty kamishina wa uhamiaji.

AM: Wow!

NJM: Na mwaka jana tu mwezi wa June tarehe 25 nimestaafu rasmi, kwa hiyo mimi sasa ni mstaafu ambaye nimefanya kwenye idara ya uhamiaji kwa miaka 41.

AM: Hongera sana.

NJM: Asante.

AM: Kwa sasa kazi yako inaonekanaje, najua ulifanya uhamiaji lakini je sasa huko kwenye michezo? Unaweza kusema nini katika kazi yako na nini unaweza sema unajivunia kama mafanikio yako makubwa katika kazi yako.

NJM: Kwaanza niseme nashukuru idara ya uhamiaji Tanzania, kwa sababu haikuwa kikwanzo kwangu katika kuperform kwenye michezo. Mimi katika hiyo idara ya uhamiaji nimepata sapoti kubwa sana ya kushirika katika michezo kwa sababu idara ya uhamiaji moja ya sera zake katika kufanya kazi ni michezo. Na kama unafahamu kuwa vikozi vyote vya ulinzi na usalama wanamichezo yao ya kijeshi ambayo inaitwa Bamata. Kwa hiyo ilikuwa michezo ni sera katika idara ya uhamiaji, kwa hiyo nimepata sapoti kubwa sana ya kuwa niendelee kucheza. Kwa hiyo nimeshiriki michezo yote ambayo kwa level hiyo

ninayokwambia kuanzia Tanzania, East Africa, mashindano ya Afrika, mashindano ya commonwealthy, mashindano ya dunia kwenye group series nikiwa mimi ni mtumishi wa idara ya uhamiaji. Na kwa kipindi chote hicho sikuwahi hata siku moja kupata tatizo la kikazi kwa nini unashiriki michezo kwa nini kazi… kwa sababu nilikuwa naweza kujipanga kusema kweli. Nilikuwa najipanga muda wangu wa kazi na kujikita kwenye masuala ya kazi kwa aslilimia mia moja na muda amabao naruhusiwa basi natumia ule muda wa kuruhusiwa kama ambavyo inahitajika na kumaliza. Sikuwahi take advantage ya ruhusa yangu au sikuwahi take advantage ya kuwa mimi ni mwanamchezo basi nifanya vyovyote vile ndivyo si hivyo hapana. Na nimeheshimu kazi yangu na nimepata heshima kubwa na muda wote nimepeta sapoti ya viongozi wangu katika idara ya uhamiaji. Vile vile huu mchezo wa Band Minten ulifika pahali ukamalizika Tanzania, mimi niseme ulimalizika kwa sababu kama mwaka wa 93 sisi tunarudi mashindano ya dunia basi Band hall la Zanzibar liliweza kufungwa na hatukuweza tena kuendelea na huo mchezo likatumika kwa matumizi ya mashule. Maana yake ni hall ambalo lilitumika kwa shule ya Bembele ya Zanzibar. Kwa hiyo tukaambia sasa hivi halitumiki tena kwa mambo ya michezo hili linahitajika sasa kutumika kwa mambo ya mashule. Na mchezo wa Band Minten sio mchezo ambao unaweza kucheza nje, ni mchezo amabo ni lazima upate hall kwa hiyo hapo stori ya stori ya Band Minten ulimalizika kwenye 93. Kwa hiyo mimi sasa ukiwa mwana michezo unaweza kucheza michezo mingi, mchezaji mzuri yeyote yule experience inaonyesha lazima atakuwa kacheza different sports. Lakini anajikita kwenye ile best performance yake kwa hiyo wakati mimi nacheza Band Minten lakini mimi kama ninavyo kwambia nikikaa hapa napicha mpira, kwa hiyo mpira mfano pia nilikuwa nacheza football, nacheza football na ndugu zangu wa kiume tunacheza, tunacheza. Mwaka 88 ilikuja team ya football ya wanawake kutoka Sweden Tanzania ilikuwa inatua na Zanzibar ilikuwa inakuja. Inaitwa Teresio inatoka Sweden na hapa Zanzibar ilipokelewa na UWT Zanzibar umoja wa wanawake Tanzania ile ya CCM Tanzania ukapokelewa wale wageni kwa hiyo walitukusanya sisi wana michezo kucheza match Amani very professional Stadium ambayo ni kubwa Zanzibar kipindi hicho kama ninavyokwambia na wanawake kwa mara ya kwanza tukapata fursa ya kucheza mchezo huo hapo Amani Stadium. Kwa kweli mwanzo mgumu na kwa sababu ulikwa sio team ni wachezaji ni wana michezo mbalimbali walikusanywa tuliweza kuperform kukidhi ile haja ya kuwa kwa kuwa wamekuja wageni na tuonyeshe spirit ya sports. Kwa hiyo tulicheza na baada ya hapo sasa kwa sisi ambao tulijikusanya baada sasa ya ile match tukaendelea sasa kucheza football team ya wanawake. Kuanzia 88 nilikuwa pia nacheza football ya wanawake na huko ni mchezaji wa Band Minten. Tuliendelea hivyo mpaka nimeweza kucheza national team ya Tanzania kwenye mashindano ya kwanza Africa ambayo Tanzania imeshiriki women football mimi nilishiriki. It was 2001 lakini by that time tena umri wangu ulishaenda kwa hiyo mimi ilipofika 2005 na kwa saabu siwezi tena kucheza kwa kiwango kikubwa kutokana na umri wangu nikaingia mambo ya kusomea coacher foodball coaching. 2005 mpaka hivi sasa ninavyokwambia mimi ni coacher ambaye nimefika level ya leseni A Tanzania na afrika na ni instructor wa CAF wa Afrika na vile vile nilikwenda kusoma UEF kule Germany DFB nina leseni kutoka Germany. Kwa hiyo mimi sasa hivi ni coacher niko kwenye masuala ya football kama coacher instructor coach ambayo hata juzi tu nilikuwa Tanga kwenye refresher course ya class A leseni amabayo ambayo ilitayarishwa na CAF. Hii week iliyopita kabla ya ramadhani, kwa hiyo pia baada ya kuacha Band Minten nikawa kwenye football nimefundisha team ya taifa Tanzania taifa stars nilikuwa kwenye team kwa miaka 6, miaka

minne nikiwa assistant coach chini ya coach wawili maarufu ambao ni Mkwasa na Kaijage wale ni macoach ambao mimi nimefanya nao kazi nikiwa coach msaidizi. Lakini nikawa coach kwa miaka miwili kwenye Twiga stars Tanzania kutokana na kazi yangu sasa, kama nilivyo kwambia nilikuwa depty kamishina maana yake ni cheo cha juu sana katika wizara ya mambo ya ndani idara ya uhamiaji. Kwa hiyo ilifika pahala sasa ikawa majukumu ni mazito ni makubwa muda haugawiki tena kwenda kwenye private sectors kushughulikia mambo kama hayo kwahiyo, nikawa full participating kwenye masuala ya kazi kwa hiyo kule Twiga stars nikaachana nayo kwanza kwa level ile na mimi niendelee kuangalia maisha ya kazini. Kutokana sasa na majukumu mazito ambayo yalikuwa na dhamana kubwa sana ambayo sasa kwangu mimi nisingeweza kujigawa sana nikaona vitu viwili vinachaguliwa sasa kutulia kwanza kazini. Lakini kwa kweli muda wote mimi nilipata sapoti kutoka kazini kwangu. Asante.

AM: Asante sana kwa maelezo hayo. Inapokuja historia ya maisha yako na kazi, mengi umeyaongelea lakini naomba nikuulize machache ni nini kilikuhamazisha katika kazi unayoifanya. Maana yake hapo naona kama kuna kazi mbili kuna hii ambayo umeajiriwa nayo kwenye wizara ya uhamiaji alafu bado kuna hii masuala ya michezo.

NJM: Kwa kweli kazi yangu kwenye wizara ya uhamiaji nikiuzungumzia mimi ni kazi ambayo niliipenda sana na niliifanya kwa juhudi zote. Ni kazi ya kutoa huduma kazi ya idara ya uhamiaji unatoa huduma kwa watu ambao nakuhakikishia kuna watu milion moja Zanzibar basi wote wananijua. Kwa kupitia huduma ya uhamiaji na huduma zingine ambao tulikuwa tutatoa, ni kazi ambayo inakutengenezea mazingira makubwa sana ya kutengeneza mahusiano na watu tofauti tofauti kwa sababu ya huduma ambazo unazitoa kuanzia raia mpaka wageni. Na bahati nzuri nimekuwa na dhamana katika sehemu tofauti tofauti, nimefanya kazi kama mkuu wa kitua bandarini, nimefanya kazi makao makuu katika vitengo mbalimbali, nimeweza kuwa mkuu wa desk la passport la kimataifa diplomatics passport. Nimeweza kuwa katika sehemu ya mahusiano, nimekuwa katika kipindi cha kutoa huduma ambacho ni mambo ya permit. Kwa hiyo, ni kazi ambayo kwa kweli ilikuwa inatengeneza nasema appearance, ile CV yako kwa jamii. Ni kazi ambayo unapata experience kubwa katika kujua maisha ambayo watu yanayaishi, historically background za watu hizo zote utazijua. Kwa sababu inakufundisha kufahamu watu ili kuweza kufanya kazi zako. Unajua majukumu yetu ya kimsingi ni kutoa pasipoti tuseme, kutoa permit lazima tujue watu ndio tuweze kutoa pasipoti. Huwezi kutoa pasipoti kinyume cha sheria cha pasipoti, na sheria yake apewe mtanzania. Sifa ya kwanza ni kupewa mtanzania lakini wewe kama hujiongezi kufahanu maisha ya watu na jamii unaweza kutoa pasipoti kwa makosa akaja mtu kweli kakudanganya na cheti cha kuzaliwa lakini pengine sio mtanzania lakini ukimuangalia tu utamjua kuwa sio mtanzania pamoja na kuwa na documents zake zile. Kwa hiyo wewe kama afisa uhamiaji unapata awareness kubwa sana experience kuishi na watu unapata. Maana yake unapata contacts za watu wengi sana interaction ni kubwa sana, communication unapata kubwa sana. Kwa hiyo ni kazi nzuri nimeipenda kwa muda wangu wote ambao nimeifanya kwa sababu imenijengea mahusiano makubwa sana na jamii imenifanya nimepata experience kubwa sana ya kudeal na watu. Kuelewa matatizo ya watu kujua ni nini hasa maisha, inatoa huduma hii kazi kwa kweli ni kazi nzuri sana. Na inatakiwa uaminifu, inatakiwa uadilifu, inafuatwa miongozo, sheria na

kanuni na taratibu ambao ukiwa katika line basi huwezi pata matatizo ya aina yeyote. Kwa kweli mimi nashukuru sana kwa kipindi changu chote, nimeondoka kazini nikiwa salama na bado ninahitajika lakini ni kweli muda hauniruhusu tena. Kwa kweli mimi nimefanya kazi halihamdulilahi namshukuru Mungu wangu.

AM: Asante sana mama Nasra. Labda nikuuulize swali la mwisho, je umekuwa na mabadiliko binafsi kutokana na kujihuzisha katika harakati? Maana yake harakati zako maana naona harakati zako zaidi zimeenda kwenye michizo

NJM: Mabadiliko makubwa niliyonayo kwanza; appearance unakuwa mwanamke tofauti kuliko mwanamke wa kawaida kwa sababu ya ile physical commision kutokana na mazoezi, sportness yako, awareness yako, kama nilivyokwambia nimeshiriki mashindano mengi kwa hiyo maana yake nimesafiri sana nimejuana na watu tofauti tofauti. Nimeweza kuingiliana na watu tofauti tofauti kwa hiyo kwa vyovyote vile siwezi kimtazamo kuwa sawa na mwanamke wa nyumbani. Hiyo moja lakini jingine nimeshika dhamana mbalimbali kwa mfano upande wangu wa kazi jeshini mimi nimekuwa makamu mwenyekiti wa Bamata, Bamata ni Baraza la michezo ya majeshi Tanzania. Sasa kwenye hilo baraza lina majeshi yote Tanzania sasa kufikia level ya kuwa makamu mwenyekiti maana yake wewe ulikuwa mtu mwenye special character. Lakini kama hiyo haitoshi Bamata lenyewe, mimi nimeshastaafu lakini katika katiba yao wameibadilisha kupitia kustaafu kwangu kwa sababu bado wana hisi huyu mtu bado tunamhitaji. Mimi ni member wa heshima maisha yangu yote maana yake whenever itafanyika Bamata basi mimi nitakuwa invited. Hata juzi nimekuwa invited kule Mtwara kulikuwa na mchezo wa Bamata nimekuwa invited kwenda kule kwa sababu ya ile heshima una members wa maisha nimewekewa. Kuanzia baada ya kustaafu mimi ndio imetengenezwa hiyo, sasa nani mwingine atapata hiyo chance lakini ujue pia kutokana na performance yako watu wanaheshimu uwezo wako ulionao. Lakini pia niseme kuwa hata kazini kwangu mimi nilikuwa kwenye kamati kuu ya michezo mimi ni katibu. Maana yake katibu ndio unaratibu masuala yote ya michezo. Kwa hiyo na wao wamenialika mimi ni member wao wa maisha yangu yote mpaka nitakapo fariki katika dunia hii, kila wakifanya mikutano vyao hivyo vya michezo kamati kuu mimi naalikwa. Maana yake nini maana yake wanakosa uwepo wako ile smartness mtu unaweza kuchangia unaweza ukatoa neno likasaidia jambo fulani. Lakini pia mimi ni member wa Tanzania Olympic committee tangu 2003 mpaka sasa miaka 20. Mimi ni kiongozi katika Tanzania Olympic committee, nafikiri unajua mambo ya michezo hayo, kwa hiyo tunadeal na michezo tunaangalia zaidi michezo Afrika na Olympic game. Kwa hiyo character hizi zimenitengeneza sana, zimenitengeneza sana kiasi ya kuwa pamoja na kuface challenges mbalimbali nikiwa kama mwanamke lakini bado nimeweza kusimama kama mimi na nimeweza kuwa active na pia nimeweza kutokea mbele ya wanaume na wameweza kuona huyu ni mwanamke jasiri lakini la pili wa vitendo sio mwanamke jasiri wa kubebwa. Uwezo wako mkubwa ulionao watu wanauheshimu sana tena sana kwa hiyo hilo sio jambo dogo, mfano juzi nimekwenda refresher coach wa A license CUF mwanamke ni mimi peke yangu kwenye wanaume 26 mwanamke ni mimi peke yangu. Lakini respect yangu ya hali ya juu naipata kwa vile ninavyojitokeza, how I perform and how I put myself. Kwa hiyo naendelea hivyo na mpaka sasa hivi hali hamdulahi mtazamo wangu ninavyojiona ni kuwa nashirikiana na watu sana nafahamiana na watu wengi sana na sijawahi kupata shida nikiwa na jambo lolote nashirikisha watu napata msaada unaositahiki.

AM: Asante sana dada Nasra unaonekana umefanya mambo makubwa sana.

NJM: Asante sana nashukuru sana.

AM: Sasa tukija sehemu ya tatu tafakari ya maisha ya kazi. Unaelewaje neno Feminia? Au Uanaharakati.

NJM: Mh! Feminia, maana yake ni uanaharakati wa kike?

AM: Ni Feminist ni ule ukombozi wa kike wa kimapinduzi

NJM: Mimi nafikiri kitu cha msingi sana ambacho sisi wanawake tunatakiwa tujielewe. Tujielewe sisi wenyewe kwanza kwa sababu kuna haki zetu ambazo tunastahiki lakinii kutojielewa tunazikosa zile haki. Lakini ukiwa unajielewa wewe ni nani msingi wako wa maisha ni vipi mimi nafikiri hata wanaume wanatusapoti. Kwa hiyo awareness public awareness muamko wa watu kufahamu mambo yanayoyahusu day to day activities ni muhimu sana. Especially kwa wanawake wote walioko rural areas mi niseme kwa sababu watu wa urban area yaan mjini wengi sana wameshapata awareness kubwa sana kuhusu maisha ya wanawake. Wengi wanasoma wanajishughulisha kwenye mamo mbalimbali, wanapata kazi, wanajiunga na taasisi, wanaingia kwenye michezo, wanaingia kwenye shughuli nyingi matamasha, bonuza. Lakini bado kwenye rural area wanawake wa vijijini wanahitaji awareness kubwa sana. Kwa sababu maisha yao bado yamebaki yeye ni mama wa nyumbani, hajui haki zake za msingi, hawezi kujitetea, hawezi kuwa na maisha ambayo yanaweza kuwa bora kwa future life maana yake yeye ni mama wa nyumbani alale aamke apike apakue akimaliza kubwa akalime shambani. Nafikiri nyie wanahabari au serikali husika bado ina kazi kubwa ya kuonyesha haki za mwanamke katika maeneo mbalimbali tofauti tofauti ili mwanamke mwenyewe kwanza ajielewe aweze kufahamu kuwa mimi kama mimi nini natakiwa kupata kama haki zangu katika maisha yangu haya niliyo nayo. Kwa hiyo nafikiri hilo ndio jambo kubwa na bado kazi ipo kwa sababu mpaka sasa bado huko ndani ndani bado kuna watu maisha bado ni ya kizamani hakuna awareness. Mwanamke hawezi kufanya michezo, mwanamke hawezi kwenda shule kusoma inga hivo bado tunapiga hatua kwa hatua. Kwa mfano kipindi sisi tunacheza mpira ilikuwa haina utaratibu tulikuwa tunacheza kama hobby tu, tunapenda lakini kwa sasa kuna utaratibu wanaenda sasa kwenye utaaluma wanawake wanaweza kulipwa kwaajili ya mpira tayari mashindano ya kidunia wanawake wanafanya, zamani huko mambo hivo huwezi kuviona. Maana vilichukua muda sisi kuja kuviona na vitachukua muda sisi kujihuzisha maana yake sasa kumbe na sisi tunaweza kujaribu. Unasikia team ya wanawake wameshiriki unaona under 17th yetu imeweza kufika world cup dunia sasa inatuona it takes time. Hii ni hatua kubwa muhimu sana lakini waanzisha mpira ni sisi, hatukupata privileges zile sisi hatukupata sasa kuna steps forward ambazo zinafanyika which is good. Sasa hizo steps forward bado ziendelee kufanyika kwa sababu public awareness inahitajika sana kwenye maeneo tofauti tofauti. Kwa mfano hapa Zanzibar kwa mfano kuna mashule kuna government schools kuna kila kitu ila mchezo wa mpira wa wanawake hauchezwi sasa where are you going to get a player, wapi utampata mchezaji aje acheze mpira. Kama kwenye level of school huwezi mpata mchezaji, hakuna involvement ya wachezaji kufanya

mazoezi kucheza mpira. Kwa sababu gani unajua; culture hulka na tabia mwanamke atandaje kule kwenye mipira sio mchezo wa wanawake. Na hiyo tayari ni trauma ambayo vipo kwenye vichwa vya wazee wetu kaka zetu, ndugu zetu, dada zetu you see. Sasa it needs to be a lot of awareness katika public na katika jamii na wala ionekane kama ni kitu cha kawaida yule mwenye uwezo afanye asiyekuwa na uwezo aache. Watu wajigawe mfanya biashara afanye biashara, kama mwana siasa aende siasa, mwana mchezo aende kwenye michezo, Mtaalam afanye utaalam, we need to do more about this. Does it make sense?

AM: It makes a lot of sense, asante sana. Swali lililokuwa linafuatia ni je inamaana gani katika kazi yako, lakini umezungumzia kwenye maelekezo yako uliokuwa umeyatoa. Sasa swali linalofuatia je una mahusiano gani na wafanyakazi wengine kazini kwako. Hiyo umeshataja kidogo labda uongezee kama una chochote cha kuongezea.

NJM: Yaan mimi nina bahati nzuri sana, ndugu yangu Meena mimi nimeondoka kazini naagwa watu wanalia sijapata kuona yaan mtu hawezi kusema analia huku akisema unaondoka tunakukosa. Mimi naitwa mama, naitwa dada, naitwa boss, naitwa mkuu, naitwa afande yaan kila mtu anavyoniita anaona hajafikia vile anavyohisi aniite ili mimi nirizike. Kwa kweli nimeondoka kazini kwangu nikiwa na mahusiano mazuri sana makubwa sana namshukuru Mungu. Nimefanya kazi na watu wengi na sijisifu lakini kuondoka kwangu kumeacha pengo kuonyesha fulani ameondoka bado halijakuwa covered. Na hayo nayasema kwa maneno yanayozungumzwa na hata hao viongozi wakuu wa Idara kabsa kabsa nimeondoka vizuri, nimeondoka watu bado wanatamani niendelee kubaki kazini, nimeondoka watu bado wanaona nafasi yangu, nimeondoka watu wananihitaji kazini. Kwa hiyo naamini nimeondoka vizuri kazini nimesaidia watu kufundisha kazi, nimewasaidia wengi kuwapa maisha. Maana unapokaa kwenye kazi wewe unakuwa ni kiongozi na kiongozi kuna watu wanakuwa chini yako jinsi unavyowasaidia kuwaongoza ukawafundisha ukawaelekeza wakafanya kazi kwa kuipenda wakafanya kazi kwa kuheshimu wakafanya kazi kwa kufuata maadili na taratibu, sheria na miongozo na wale watu wakakuelewa wakafuata taratibu zile hawawezi hawawezi kukusahau maisha. Sasa wapo watu ambao nimeondoka hawawezi kunisahau kwa maisha yao yote ya kazi. Watanikumbuka na watanikumbuka kwa sababu nimeondoka kwa mahusiano mazuri sana nimeondoka pahala ambapo naamini bado nahitajika. Mfano tu nikupe kabla ya kumaliza kazi kwa mwezi mmoja ule wa mwisho unatakifa upumzike tu wanasema retired leave. Mimi sikupata retired leave nimeombwa nibaki, mkuu tunakuomba utusaidie mpaka last minutes, mimi nimefanya kazi mpaka leo namaliza Ijuma tarehe 25 ndio siku yangu ya mwisho. Retired leave yangu imemezwa ndani ya muda wa kazi ingawa nimepewa maslahi yangu maana wamenilipa. Lakini ujue vipi walihusi kuwepo kwangu una umuhimu wake, sikufanya retired leave. Na hawakuwa na uwezo kuniombea kuniongezea kwa sababu taratibu zinabadilika sasa ukimaliza unaondoka na kweli inastahiki ukimaliza uondoke kwa sababu age nayo inatosha. Una miaka 60 ya kazi kafanye mambo mengine, kapumzike nyumbani. Nenda kajishughulishe na familia muda wingi sana miaka 41 sio kidogo. Utoto wangu ujana wangu utu uzima wangu wote umeishia kazini. Sasa ufike pahala urudi nyumbani utazame maisha mengine umalizike vizuri. Pensheni nzuri kubwa ya kutosha unaweza kukaa ukatulia ukatazame mambo ya maisha na familia na mengine. Bahati nzuri mimi niliolewa na nina watoto wawili na mtoto wangu mmoja alifariki mmoja ninae sasa

hivi yuko chuo anasoma chemical engineering kwahiyo nina mtoto mmoja alhamdulillah namshukuru Mungu. Asante sana.

AM: Hongera sana mama.

NJM: Asante sana.

AM: Hayo ni mahusiano yako kwenye kazi ile iliyokuajiri lakini kuna uhusiano kwenye hizi asasi za michezo huko umeongelea mpaka umepewa honorable membership kwenye baadhi ya taasisi. Kwa hiyo hilo ni kama umeshalijibu. Labda nikuulize una maono gani usuzani kwenye michezo huko baadae, umegusia gusia hasa kwenye masuala ya wanawake.

NJM: Tuna tatizo, tuna tatizo la ushiriki michezo wanawake wenye high performance Tanzania mi nazungumzia Tanzania lakini sio Tanzania tu liko around yaan within Africa. Wenzetu wengine wameshapiga hatua lakini bado ndani ya Africa tuna tatizo lakini ngoja tuzungumzie hapa nyumbani, tuna tatizo la performance ya wanawake kwenye high performance. Mwanamke kwenye level ya shule michezo mingine yote unampata except labda niseme ladies football, na hiyo labda so soon wanaweza kufanya involment kwa sababu ni kitu ambacho kimeshapiga hatua kama na wao wana proper league hapa maana yake nini, maana yake siku lazima wataenda mashuleni watapata wachezaji wa kufundisha ambao watakuja kufanya performance kwenye national performance team au kwenye vilabu. Sasa wanawake Tanzania ni wachache wanaoshiriki katika michezo. Na kama utakumbuka miaka miwili ya nyuma mimi nimechaguli niko kwenye kamati ya Tanzania women festival/sport festival. Women sport festival si linafanyika bara linafanyika Tanzania limefanyika mwaka juzi, likafanyika mwaka jana na hilo ni kwa agizo la mama Samia rais wetu wa Tanzania aliona nafikiri na yeye kama hebu tukusanye wanawake kila mwaka wafanye michezo ili tuone na kweli tumekusanya mimi niko kwenye hiyo kamati. Nimechaguliwa na wizara ya Sanaa Utamaduni na Michezo niko kwenye kamati hiyo. Kila mwaka tumeshafanya mara mbili nategemea na mwaka huu huu pia utaendelea na tumeanza kufanya ya kimataifa maana yake Tanzania lakini pia tumefanya kuwahuzisha wenzetu kama Kenya na Uganda. Tunataka kufanya kubwa zaidi hii ni njia moja ya kusaidia involvement ya wanawake katika michezo kwa sababu pale tunafanya michezo yote. Netball, basketball, Volleyball, ladies football and boxing, yote. Inafanyika pale kila mwaka tunafanya ila ni one step forward kwa sababu haikuwahi kufanyika kwa hiyo ina maana ile mtu ambaye ameshiriki mwaka jana, team ambaye imeshiriki mwaka jana na haikufanya vizuri mwaka huu ikitaka kushiriki si inamaana inataka kufanya vizuri. Kwa sababu tunazichukua zile best team zile top 4 teams katika Tanzania league tunawachukua. Maana yake nini, maana yake yule atajitahidi mwakani kwa hiyo mwaka huu afanye kwa maana involvement, improvements ya watu wanaotaka kushiriki kwenye performance ili wapate zawadi. Mkusanyiko ule husaidia kutuonyesha wanawake nao kumbe wapo na wanafanya michezo. Lakini pia kama unavyo iona sasa kama nilivyokuambia league ya Tanzania sasa hivi under 17 wamefika world cup haikuja from nowhere ile kuanzia mwaka 2013 tulianza kushiriki 2013 tulianza kushiriki Tanzania tukianza kushirikisha team ya watoto wadogo wanawake. Ambao 15 walikwenda airtel rising star tournament ambayo ilifanyika Nigeria, watoto wetu wa under 15 waliuchukua ubingwa Africa hao ni walikuwa wanawake. Ndio

hawa sasa wanaofanya vizuri kwenye Twiga Star tukasema senior team ile ndio wale, tulitoka nao huko kwenye 15 ambao walishiriki airtel rising star walishiriki mashindano Nigeria wakachukua ubingwa Africa. Ndio maana ukaona Tanzania ilifanya vizuri football, tuliwachukua mbali sana, kutoka 13 huko 2013 wamekuja kufanya performance huku baada ya miaka minane-saba kumi umeshafahamu mpaka sasa hivi ndio mabingwa. Sasa ukiwekwa msingi ya development, tuna short term na long term. Short term ni ile wako tayri vizuri wanaenda kushiriki, long term ni kuwatayarisha, lazima kuwe na long term program kuwatayarisha from grassroot level kuwatrain kuweza kuwa groom. Kwa sababu performance ya michezo kwa mtu kuja midalest ni ten years hakuna shortcut kuanzia miaka kumi yuko kwenye training hakuna shortcut. Kwa hiyo kwenye vyama vyetu vya michezo hivi nakumbuka hata sisi kwenye TOC ile tunataka kila chama cha michezo kuwe na women kwenye committee. Kila kwenye association kuna female committee, kwanini kuwe na women committee sababu wanawake watakereka na maendeleo ya wanawake wenzao. Watataka kujua kwenye mchezo huu wanawake wanafanya nini, lakini vyama vinashindwa hakuna women committee unaweza kukuta kwenye leadership kwenye viongozi 40 kuna wanawake 3 hiyo ni weakness. Kwenye hizo association, kwenye michezo vyama labda 45 Tanzania nzima wanawake unaweza wakuta ni 3-4 au 5 hiyo sio sawa. Sababu ni nini hakuna zile program za kuwaendeleza hadi waje wapate huyo kiongozi, hakuna hiyo program ya kumleta huku hadi ukampata huyo kiongozi. Kwa hiyo hivyo ndivyo vitu vinatakiwa vifanyike kuwe na basic preparations from grassroot level kwa watoto mpaka wafikie level za juu tuende nao. Kama ninavyokwambia kwenye high performance hapo hakuna kwa sababu kwenye performance ya shule mtu anacheza mpira anacheza netball anacheza basketball anacheza riadha kutokana na matakwa ya shule. Akimaliza kutoka kumaliza shule anaacha huyo hata kama alikuwa mzuri vipi kwa sababu hakukukuwa na kitu kinamgusa akimaliza pale anaenda zake kuolewa anazaa maisha yanaisha. Sijui umepata hiyo picha, kwa hiyo sasa kuna kazi kubwa sio ya serikali peke yake sio ya wizara husika na michezo lakini zinazo husika na maisha hasa ya watu binafsi awareness hiyo na maisha ya vyama vya michezo na ya groups za michezo na maisha ya vilabu vya michezo. Maisha ya viongozi wa michezo this is involving everyone is not about taasisi fulani tu mfano wizara ya utamaduni na michezo au wizara ya utamaduni…. Haiwezekani. Lazima uwe kuna wasaidizi kuna watu wameandaliwa kwenye level ya chini wamekuja juu. Nafikiri hiyo ndio concern iliyopo kwa sasa na kwa hakika tunaenda step forward kwa sababu kama mheshimiwa rais Samia Hassan anasapoti michezo asilimia moja na yeye ni mwanamke na kama nilivyokwambia yeye ndio ameanzisha hiyo Tanzania women sport festival kwa hiyo sio jambo dogo hili. Sasa hivi anafanya vizuri anasapoti michezo mpaka wanaume wanfanya vizuri. Si unaona hizo anatoa geret Twiga star hao under 17 wa Tanzanite wote amewatunza kwa hiyi ile ni motivation haijawahi kutokea. Marais wa nchi hii wote waliowahi kuwepo haijawahi kufanyika. Mwaka wa 80 mimi niliwahi chaguliwa Tanzania mwanamchezo bora wa kike nakumbuka siku zile marehemu rais Benjamini Mkapa ndio aliyekuwa waziri wa Habari Utamaduni na Michezo alinipa mimi zawadi kama mwanamchezo bora wa mwaka 1980. Nilivyochukua world award for Africa kwa wanawake, sasa lakini nimetoka wapi mpaka nilikwenda kuchukua ubingwa wa Africa wa wanawake, nakupa mfano maana yake nimetoka wapi mimi mpaka nikaenda kuchukua ubingwa wa watoto wa kike Africa under 20th nimetokea wapi? Nani alinitayarisha sijui kama unafahamu point yangu. Kwa hiyo tunaopenya ni wachache kutokana na awareness na mazingira ya maisha yetu unapata sapoti ya mama yako baba

yako yaan family support. Lakini kama hupati sapoti hufiki huko. Sasa mimi nimechomoza kwa sababu kwetu sisi mimi nilikuwa na full sapoti ya familia. Baba yetu mama yetu, baba yetu sisi zamani tukiwa wadogo tunasafiri tunakuja Dar es Salaam kwenye michezo ya wahindi anatuleta yeye mwenyewe anakuja tunacheza anatuona hivi kakaa kwenye viti anatutazama. Tukimaliza michezo anaturudisha nyumbani watoto wake wadogo sasa sapoti kama hiyo sio kila mzee anayo kwa hiyo mimi sikutoka from nowhere mpaka nikachukua ubingwa Africa ile 79 lakini nimekuwa under preparation under family support nimepewa kutoka chini. Sasa vitu kama hivyo lazima viwepo na awareness ya namna hiyo. Mimi nafikiri ni hayo kuwepo na a lot of awareness kuweza kusapoti watoto wao waweze kuperform society inahitaji awareness.

AM: Sawa sawa, nashukuru, Naona kwenye swali la nne ni kama umeshaliongelea mahusiano ya feminia na harakati zako. Je nini mtazamo wako kati ya Feminia na Uharakati kwa ujumla na katika kazi yako. Umegusia gusia nini unachofanya kwenye kazi zako hasa za michezo, jinsi ya kupromote wanawake waingie kwenye michezo umeongelea hivyo committee kuhakikisha wana wanawake wa kutosha. Umeongelea jinsi kuwe na sehemu husika ambazo zitakuwa zinaendeleza vipaji vya watoto wa kike, hususani wanapokuwa mashuleni kuendelezwa transition hiyo. Kwa hiyo kama kuna chochote cha kuongezea unaweza kusema.

NJM: Mimi nafikiri kwetu Tanzania tuna vipaji vikubwa sana vya michezo tofauti tofauti na michezo ni gharama any mchezo lazima uwe na gharama. Sasa lazima wizara husika za michezo waendelee maana yake wanafanya, waendelee kujitahidi kutoa sapoti nchini kujua kuna matatizo gani . Naona sasa hivi kuna mabadiliko makubwa sana tangu aonekane mheshimiwa rais anasapoti michezo hata wale wenye harakati kwenye maeneo ya kazi pia na wao sasa wamebadilika. Mode zao zimebadilika wanakwenda kabsa wanashuka chini maeneo kabsa kuangalia maeneo nini kinafanyika, na hata hivi juzi tu kwa mara ya kwanza mpira uliteuliwa na baraza la mpira wa taifa kama ulisikia tumetoa zawadi kwa wanamichezo bora na mimi ni mmoja kati ya mjumbe wa kamati ile. Ile ni mojawapo katika motivation, haijawahi kufanyika tangu uhuru wa Tanzania ufanyike maana yake. Hapa ndio kwa mara ya kwanza tumekusanya watu wa michezo yote na kusema huyu alileta sifa gani, huyu alileta sifa gani, tuwapeni zawadi ya motivation. Tunataka watu watambue kuwa unajua hapa nafanya hivi pengine nitapata mwanamchezo bora vitu kama hivyo vinahamazisha sana kuwavuta wachezaji mbalimbali. Kuna kitu nitafanya makosa makubwa sana kama sitakukwambia. Mimi nina vitu vingi sana wakati mwinging vya muhimu lakini kwa kuwa nimekumbuka hapa nitakwambia hapa hapa. Mimi nimepewa tuzo na marais wawili wa Tanzania. Tuzo ya mwananchi rais wa Zanzibar rais mwana mapinduzi aliyewaletea sifa Zanzibar nimepewa hiyo tuzo na rais wa Zanzibar kupitia michezo. Nimepewa tuzo na mheshimiwa rais Sheinya mfanyakazi uliyotukuka, mfanyakazi bora uliotukuka wa muda mrefu. Kuanzia mimi nina tuzo mbili moja nimepata kwa rais wa jamhuri wa Tanzania mama Samia na nyingine nimepata kwa rais wa serikali ya mapinduzi wa Zanzibar Dr. Shein. Nimepata hiyo moja kwenye sherehe za mapinduzi ya miaka 50 nilipata 2021 zilitolewa kwa utumishi uliotukuka na wa muda mrefu na hizo hizo tuzo. Sasa kufikia idara yako, kwa sababu its not from nowhere haiwezekani tu kuwa rais atamchagua mtu pap kuna watu wamefanyia kazi mpaka ukafikia pahali watu wakasema yule anafaa. Kwa hiyo nakubebesha ule mzigo uone vipi ilivyokuwa maana yake mpaka top level ya

serikali marais wameweza kunitunza, nina tuzo mbili ambazo nimepewa na ninazo. I'm very proud of myself na nimeziweka nilikuwa nazivaa sana mwenyewe nilipokuwa kazini lakini sasa hivi tena nitazivaa siku zingine. Lakini pia nazivaa sana kwenye mikutano mikubwa mikubwa oficial nazivaa zile maana ni medali zangu. Sasa ninachotaka kusema ni kuwa tujitahidini tufanye vizuri tuwe na uzalendo, tuwe watu ambao tunaumia na maendeleo ya nchi yetu ili ifikie pahala watu wengine waone kuwa huyu amechukua juhudi binafsi. Huyu amefanya jambo hili kubwa na ndio maana ikafikia level ya kupewa tuzo na marais wawili wa nchi hii sio jambao dogo. Kwa hiyo hilo ndilo neno nataka kulisema tuweni mifano ya kuigwa, watu wengine wayaone hayo kama ni mazuri watamani na wao kufikia kwenye level kama hiyo. Lakini haiji kiurahisi lazima kuwe na full commitment ya kujitahidi na kuona juhudi binafsi uzitie ili uweze kufanya vizuri. Kwa hiyo ni vitu ambavyo lazima kuwe na ile mode ya kujitolea zaidi. Sikufanya vitu hivyo vyote mimi nikitegemea nikifanya hivi nitalipwa nikifanya hivi nitapata pesa nikifanya hivi itakuwa hivi. Mimi nimefanya hivi kwa hisia zangu binafsi nilizokuwa nazo nataka maendeleo nataka kitu vizuri nataka kufanya jambo nzuri kwa nchi yangu. Nilitaka kuona nimefikia malengo haya bila kujali kitu kingine kinachokuja katikati hapo. Kwa hiyo hayo ndio mambo ambayo ni vizuri watu wengine kuona ni mfano wa kuigwa tukaweza kupata viongozi ambao wanaweza kuja kusukuma nchi hii baadae. Maana yake sisi wakati wetu unakwenda hivyo, muda wetu ni kama ni asubuhi inaanza sisi tuko jioni.

AM: Mko mchana bwana haha da Nasra bwana.

NJM: Tuko jioni, kuna mtu akaniambia "kama nina uwezo natamani nirejeshe miaka 20 nyuma ili urudi immigration uje ufanye kazi na sisi". Nikamwambia haiwezi tena kubadilika tumuombe Mungu atupe uhai na uzima tukiwa na jambo tutaulizana tutasaidiana lakini kurudi muda haurudi. Time is killing us, asante sana my dear.

AM: Asante sana. Labda nikuulize swali moja tu kwenye hapo hapo. Ni nini ambacho unaweza kusema unajivunia kwenye masuala ya michezo hususani kwenye kusukuma watoto wa kike kuingia kwenye michezo.

NJM: Mimi najivunia maana naweza sema mpaka niliunda team ya wanawake ya kucheza mpira inaitwa Women Fighters na imecheza mpira kama utakwenda kwenye youtube ukatafuta Zanzibar soccer queen, tumecheza mpira mpaka tumeend anje hata kutembelea mataifa mbalimbali. Kwenye youtube tafuta Zanzibar Soccer Queen utaniona na kupata historia ya Women Fighters.

AM: Okay.

NJM: Kwa hiyo nimeweza motivate wanawake, niliunda team hiyo na nikwambie ukweli hiyo team niliyounda imekaa kwa muda mrefu sana hivi juzi tu 2020 na COVID hii ndio watu wametawanyika. Hata leo nikiita watakuja vipi coacher kuna nini, lakini wachezaji wangu wote nakwambia wote wameajiriwa kwenye vikosi wamepata ajira wote. Wako kwenye vikosi na wamepata ajira kwa sababu unajua ni nini unajua, wamekuwa wanamichezo wazuri wako active wako vizuri wote, sina mchezaji mpaka nasema team yangu imekufa, nasema imekufa kwa sababu sina wachezaji ndio kama ninavyokwambia

sina wachezaji. Ndio kama nilivyokwambia umetoka na wachezaji umetoka nao mbali ila sasa hivi mimi nimeshakuwa mtu mzima siwezi tena kuwafuatilia kama vile nilivyokuwa nawafuatilia mwanzo. Nimewaachia watu wengine waendeleze kujitoa ni kitu kikubwa sana sio kila mtu anaweza kujitoa wengine hawawezi kujitoa.

AM: Ni kweli.

NJM: Sio kila mtu anaweza kujitoa wengine hawawezi kujitoa. (Niko kwenye interview na redio kidogo baada ya hapa nitakupigia) Umesikia Meena sio kila mtu anaweza kujitolea mimi nimeacha team imekamilika kila kitu lakini ninavyokwambia baada ya hii COVID hii watu wametawanyika tawanyika. Mpaka roho inaniuma kwa sababu historia yangu inaanza kufifia kwenye women football kwa team yangu ile. Kwa hiyo hiyo team yangu sasa hivi imetawanyika watu wametawanyika, wameajiriwa, sasa natakiwa nikafanye kazi ya ziada kuwakusanya tena grassroot kuwatafuta ni kazi ngumu sana. Kwa hiyo nimewashawishi watu nimeweza kufundisha nimeweza kuwasaidia mpaka level ya kuweza kuajiriwa kwenye vikosi na sehemu tofauti tofauti wapo na wanaendelea na maisha yao. Na pia nimekuwa katika chama cha mpira wa miguu hapa Zanzibar football federation mimi ni mmoja wa member katika technical committee ambayo technical committee inasimamia michezo yote ya wanaume na wanawake. Na kwenye hiyo kuna kamati ya kuendeleza soccer la wanawake mimi niliwahi kuwa mwenyekiti wa hiyo kamati kwa zaidi ya miaka kumi nyuma yaan ten years zaidi, kwa hiyo pia tumesimamia hilo. Sasa hivi niko kwenye technical committee lakini bado tunawasapoti na tunawapa mbinu mbali mbali waweze kuendeleza soccer lao mbele. Kwa hiyo tunaendeleza tunawasaidia kifikira tunasaidia kuhamazisha, tunasaidia kuonyesha kuwa michezo kuna faida na ukiweza kushiriki kuna mambo mengi unaweza kupata bila kutegemea. Maana yake unaweza kupata kazi unaweza kupata marafiki unaweza kutembea, unaweza kupata tuzo, unaweza kupata hata utajiri, ninasema utajiri maana watu wanaweza kupata utajiri kupitia michezo kwa hiyo michezo ni kila kitu na tunaendelea kusema hivyo tunaendelea kuhamazisha hivyo. Kwenye Tanzania Olympic Committee kwenye ile women committee mimi ni chairperson ni mwenyekiti wa ile committee kwa hiyo pia bado nasimama kwenye level kubwa sana kuhamazisha nini kifanyike Tanzania kwa ajili ya michezo ya wanawake na ndio maana kama umeona miaka miwili sasa Tanzania Olympic imekuwa ikifanya mashindano yake personally ya kuhamazisha michezo tofauti tofauti.

Ni fikira zetu kuhamazisha na kujaribu kufanya involvement ya wanawake kuingia kwenye michezo. Kwa kweli ni mambo ambayo hayahitaji jitihada za mtu mmoja lakini tunajitahidi kwa uwezo wetu na maeneo yetu tulionayo kuhamazisha kwa kweli. Kwa hiyo kwenye leadership niko huko na kwenye kuhamazisha nimekwambia niko kwenye Tanzania Olympic Committee ni chairperson kwenye women committee. Huko Zanzibar football federation mimi ni member katika technical committee, technical committee ndio inayosimamia mpira wote, kwenye BAMATA nilikuwa makamu mwenyekiti BAMATA ni michezo hiyo, baraza la michezo majeshi Tanzania. Kwenye idara yangu ya kazi ni katibu nilikuwa kamati kuu ya idara ya michezo ambayo hiyo ndio yenye maamuzi yote nini kifanyike katika idara kwa hiyo kwenye level hizo zote ujue kama nimejitahidi kutoa mchango wangu kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya wanawake na wanamichezo kiujumla kwa ujumla wake.

AM: Okay. Sawa sawa, baada ya kusema hayo inaunganika na eneo letu la tano ambalo ndio tunakaribia kumalizia. Linasema mwingiliano wa kazi yako pamoja na mtandao wa wanawake nchini na kimataifa je unamahusiano yeyote ya mtandao wa wanawake hapa nchini Tanzania na nje ya nchi?

NJM: Kwa kweli sina, sina involvement ya moja kwa moja kwenye mitandao apart from hayo niliyokuhadithia sina involvement ya moja kwa moja. Labda baraza la michezo Tanzania lile baraza lao lile la TWF wao wamenihuzisha kwa hiyo ni mjumbe katika kamati ile ya Tanzania women festival na kama sasa hivi nimeteuliwa niko katika hiyo members wa kuteua wanamichezo bora Tanzania lakini moja kwa moja kama niko involved kimataifa ama ndani ya nchi apart from that hapana.

AM: Sawa

NJM: Na pengine hiyo imekuja sina involvement kubwa sana kutokana na nature ya kazi yangu na cheo changu nilichokuwa nacho. Nafikiri ilikuwa huwezi tena kuwa kwenye interaction na vitu vingine zaidi kutokana na maadili ya kazi na level yako ya kazi. Kwa sababu mimi sikuwa huru mimi nilikuwa ni muajiriwa kwa hiyo nilikuwa na limitation katika involvement kwa hiyo hiyo pengine imechangia kunilimit. Lakini sio kwa limititation ya kuwa siwezi tena kuchangia ila hata hizo contacts sikutaka mwenyewe kutokana na life style yangu.

AM: Okay. Sawa ingawa umeinteract sana kwenye ulingo wa michezo.

NJM: Ehe! Umeonae hiyo na kama Africa niko kwenye group la makocha kuna CAF maana yake CAF ni confederation Africa football, kuna panel ya viongozi Africa nzima niko kwenye hiyo panel vile vile. Lakini we discuss about coaching ndio niko kwenye hiyo panel ya CAF instructors especially wanawake kwa hiyo niko kwenye hiyo panel .

AM: Okay. Sawa kwa kumalizia hili ni kama lile la nyuma muunganiko wa kimataifa na aina za harakati unazozifanya hapo umeshanijibu.

NJM: Ndio nimeshakujibu, mimi nina limitations kutokana na kazi nilizokuwa nafanya kuweza jihuzisha na mambo hayo zaidi. I was not free maana yake.

AM: Lakini bado umeweza fanya mambo mengi sana kwenye sector ya michezo. Okay mama Nasra nikushukuru sana kwa muda wako, najua una mafua yamekubana pole sana lakini nakushukuru. Nashukuru sana kwa kujitoa kwako.

NJM: Na mimi kwa kweli niseme asante sana hii ni fursa Anneth, umenisaidia sana kuweza kusema watu wengine watanisikia ni fursa kubwa na mimi nakushukuru sana. Na pengine nilikukwaza kwa namna yeyote ile naomba uwe kwenye hali ya kawaida ujue tu kwamba majukumu ni mengi na kila mara nilikuwa nakuingilia kwa mambo mengine lakini kwa kweli nia ni nzuri na tuendelee kushirikiana, tuendelee kusapotiana, na sasa kama utaniingiza kwenye mitandao ya kimataifa na connection na mambo ya michezo niko tayari

maana niko free sasa. I'm free to be involved with maana yake. Inshallah mimi nakushukuru sana kwa kunipa fursa maana hii ni fursa ambalo wengine wameikosa nimeweza kuipata, nakushukuru sana.

AM: Asante sana

NJM: Nategemea fursa hii itatumika vizuri kuninyanyua zaidi, nakushukuru sana.We will keep in touch basi.

AM: Asante sana, naomba ile form unisainie basi.

NJM: I will do that Inshallah.

AM: Okay. Asante na uwe na siku njema.